NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

1 Novemba 2022

Kwa Wafuasi wa Bahá'u'lláh nchini….

Marafiki wapendwa sana,

Mpango wa Miaka Tisa hivi sasa unaendelea. Mafanikio ya kipekee ambayo mnaleta kwenye hatua hii ya Mpango Mtakatifu inaiweka jumuiya yenu kwenye safu za mbele za jumuiya ya Kibahá'i ya ulimwengu mzima. Mbele yenu imefunguka njia ya uwezekano mkubwa, na tuna imani kwamba mpo tayari kuvuka yale ambayo mmeyafanikisha hadi sasa.

Nchi yenu imebarikiwa kwa mchanganyiko wa ajabu wa makabila na tamaduni. Kiasi gani tumekuwa na furaha kwa miaka mingi kuona upokevu wa watu wake kwa mafundisho ya Bahá'u'lláh. Bado, ole, nchi yenu mara kwa mara inakumbwa na mizozo miongoni mwa baadhi ya watu wake. Kama sehemu ya jamii ya …, bila shaka, hamjakingwa dhidi ya nguvu ambazo zinatengeneza na kusukuma mgogoro. Kile ambacho hili linahitaji ni uangalifu wa waumini wote katika kuhakikisha kwamba migawanyiko, hasa ile inayohusiana na ukabila, haiweki mizizi katika jumuiya yenu. Migawanyiko kama hiyo inaweza kuzuia juhudi zenu za kuendeleza jumuiya yenu na kukuza maendeleo ya kiroho na kimwili ya taifa lenu. Wajibu wenu kama Wabahá'i ni kutenda kama mabingwa wa kweli wa umoja wa binadamu, na kuendeleza umoja katika jumuiya zenu na katika maisha ya taifa lenu. Ni kuhusiana na jukumu hili muhimu kwamba tunapenda kuzungumza nanyi.

Kila moja ya mamia ya makundi ya kikabila katika nchi yenu lina historia ndefu, na kila moja hatua kwa hatua limebadilishwa na kuumbwa upya kwa kukutana na makundi na tamaduni zingine katika vipindi vyote vya amani na migogoro. Ruwaza kama hiyo, bila shaka, siyo ya kipekee kwa ….. Ni historia ya watu wa ulimwengu, uhalisia ambao kwake mtazamo wa kihistoria wa Kibahá'i hutoa mwangaza mwingi zaidi. Kama kundi la kipekee likualo kama viumbe hai, jamii ya binadamu imepitia hatua za mabadiliko ambazo zinafanana na hatua za uchanga na utoto katika maisha ya kila mwana-jamii wake. Migawanyiko na migogoro ambayo imeainisha uhusiano miongoni na ndani ya watu mbalimbali ni tabia za utoto za jamii ya binadamuu. Katika hali isiyobadilika wala kuzuilika, hata hivyo, jamii ya binadamu imekua ikipiga hatua mbele kwenye njia ya ukomavu wake. Kwenye njia hii, jamii ya binadamu, kutoka zama moja hadi inayofuata, imepokea msukumo kutoka mfuatano wa ufunuo mtakatifu uliotumwa na Mungu ili kwa uendelevu kuielimisha na kuistaarabisha. Jamii ya binadamu sasa ipo katika nyakati za mwisho za kipindi chake cha ujana chenye misukosuko na inapitia kipindi cha mpito. Ikiwa kwenye kizingiti cha zama zilizosubiriwa kwa muda mrefu, mahitaji yake hayatimizwi tena na mawazo na tabia za hatua zilizotangulia.

Bahá'u'lláh amekuja kwa binadamu katika kipindi hiki cha ujana wake, chenye uhitaji wa ukomavu. Kama mnavyofahamu vyema, Ametoa njia kwa ajili ya kusimamisha Umoja wa binadamu, alama ya ulimwengu mkomavu. Kile kitakacho unganisha mioyo ya watu wote pamoja ni nguvu ya Neno la Mungu. Neno hilo lina nguvu ya kiutendaji ambayo katika kila zama imetoa njia kwa ajili ya kuboresha tabia za binadamu na kupangilia upya masuala ya kibinadamu. Dhima ya Wabahá'i ni kujifunza kutumia ufunuo wa Bahá'u'lláh katika maisha yao binafsi na ya pamoja na katika maisha ya jumuiya yao. Kupitia juhudi zilizopangwa vyema na kwa ushirikiano na watu wengine wengi waliojitolea kwa ajili ya uboreshaji wa ulimwengu,

Wabahá'i wanaleta kanuni zinazoendana na zama za ukomavu wa jamii ya binadamu ili kuendana na hali za watu wa ulimwengu. Wanajibidiisha kwa ajili ya mabadiliko ya uhalisia wa ndani na nje wa maisha ya binadamu, na kwa ajili ya kukuza hali za kiroho na za kijamii ambazo zitazalisha aina mpya ya watu na jamii mpya itakayosimikwa kwenye msingi wa umoja.

Wabahá'í hutekeleza kazi hii kwa kutumia vyombo na njia zinazofaa katika ujengaji wa ulimwengu ulioungana. Siku zote wanafahamu kuwa umoja siyo lengo pekee wanalolitafuta bali ni njia kuu ya ujemngaji wa jamii mpya na komavu. Wao kwa hiyo, hufanya kazi pamoja "kwa safu zinazofuatana", "moja imefungwa kwa inayofuata, kila mmoja akisaidia wenzake". Wamejipamba kwa nia safi, shabaha za dhati na mioyo aminifu. "Wanashirikiana na watu wote na ndugu wote wa duniani kwa furaha na shangwe", wakiwa na uhakika kwamba "ushirikiano wa karibu na watu umeendeleza na utaendelea kuendeleza umoja na upatano". Wanajitahidi kulinda matendo yao kutokana na ukatili wowote wa kinyama au chuki na daima hutafuta "kushikilia kwa uthabiti kwenye kamba ya wema na huruma". Zaidi ya yote, wanafahamu kwamba "Dini ya Mungu ni kwa ajili ya upendo na umoja" na kamwe isiwe chanzo cha uadui na mafarakano, na kwamba "njia za utaratibu" hazipaswi kamwe kuwa "sababu ya mkanganyiko", au "chombo cha muungano kuwa nafasi ya mafarakano".

Ni kama tu jumuiya moja iliyoungana ndipo mtaweza kujibidiisha kama waendelezaji wa umoja wa jamii ya binadamu. Hivyo, kwamba ni muhimu muendelee kukuza uelewa wenu wa jinsi gani vikwazo kwa umoja hutokea katika jamii. Tungependelea kujadili juu ya vikwazo viwili vya namna hii: upotoshaji wa utambulisho wa binadamu na ueneaji wa ubaguzi, hususani ubaguzi wa kikabila.

*

Kwenye kiini cha migawanyiko katika jamii hii leo ni janga la utambulisho. Jinsi ambavyo watu hufikiri kuhusu wao ni nani na namna waoinavyo nafasi yao katika ulimwengu huamua namna wanavyohusiana na wengine na kile wanachojali kama kusudi lao binafsi na la pamoja. Kwa Wabahá'i, ni Mdhihirishaji wa Mungu, Sauti ya Mungu kwa ulimwenguni, Ambaye ndiye hutafsiri asili na kusudi la binadamu. Bahá'u'lláh hueleza kusudi la maisha ya mwanadamu kama kimsingi ni lenye asili ya kiroho. Ukweli halisi wa mtu binafsi unapatikana katika nguvu za roho, ambazo zina uwezo wa kumjua Mungu na kuakisi sifa zake. Roho haina jinsia, haina ukabila, haina mbari. Mungu haoni utofauti miongoni mwa wanadamu isipokuwa tu kuhusiana na juhudi fahamivu za kila mtu ili kutakasa roho yake na kuonesha nguvu zake zote. Mbele za Mungu, wanadamu wote ni wamoja na wana wajibu wa pamoja wa kumjua na kumwabudu Yeye na kuchangia kwenye maendeleo ya ustaarabu. Ukweli huu unahusiana moja kwa moja na mwingine – kwamba binadamu ni familia moja. Bwana Mwenye upendo "aliwaumba wanadamu wote kutokana na asili moja". Yeye "aliamuru kwamba watu wote wawe sehemu ya kaya moja". "Kwa kuwa Tumewaumba wote kutokana na kitu kile kile kimoja", Bahá'u'lláh alisema, "Inawapasa kuwa kama roho moja, kutembea kwa miguu ile le, kula kwa mdomo ule ule na kuishi katika nchi ile ile, kwamba, kutoka katika nafsi yenu ya ndani kanbisa, kwa mwenendo na vitendo vyenu, ishara za umoja na kiini cha kujitenga viweze kudhihirishwa".

Nguvu za roho ya mwanadamu zimedhihirishwa katika historia na sayari nzima kwa namna nyingi za desturi, elimu na utamaduni. Mchanganyiko huu huijalia familia ya jamii ya binadamu utajiri. Kama vile maua ya rangi mbalimbali huitajirisha bustani, mchanganyiko huipa jamii uzuri na nguvu za asili. "Tazama", anafafanua 'Abdu'l-Bahá, "maua ya bustani: licha ya kutofautiana katika aina, rangi, muundo na umbo, bado, hurutubishwa na maji ya chemchemi moja, kuhuishwa na pumzi ya upepo mmoja, ikitiwa nguvu na miale ya jua moja, mchanganyiko huu hukuza ubora wake, na huongeza uzuri wake". "Kwa namna hiyo hiyo,"

Yeye anaongeza, "pale ambapo fikra, mwenendo na tabia tofauti vinaletwa pamoja chini ya nguvu na ushawishi wa asasi kuu, uzuri na utukufu wa ukamilifu wa mwanadamu vitabainishwa na kudhihirishwa.” Umoja katika anuwai, siyo mfanano, hivyo hilo ndilo neno la tahadhari la mafundisho ya Bahá'u'lláh.

Walakini fikirieni jinsi kikwazo kikubwa na kibaya zaidi kwa umoja wa familia ya binadamu kinavyowasilishwa kutokana na kushindwa kuelewa ukweli wa asili yake ya umoja! Hisia yoyote ya umoja inayotokana na utambulisho wa pamoja wa kikundi inakuwa chanzo cha mizozo na wale wanaochukuliwa kama “wengine". Binadamu wamegawanyika katika makundi yenye maslahi yanayoshindana, wengi wamejifungia katika mapambano kwa ajili ya kutawala. Mitazamo ya maslahi yanayokinzana huzuia uwezo wa pamoja wa kubadilisha hali za kijamii na kukabiliana na changamoto kwa ajili ya manufaa ya wote. Katika nyanja za kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi za maisha, mizozo inayochochewa na maslahi finyu binafsi huchukuliwa kuwa ya asili na isiyoepukika. Uhasama baina ya vikundi huwadhuru wote, huzuia haki na hukandamiza uwezo wa watu binafsi na vikundi, ambao michango yao ni muhimu kwa ajili ya uboreshaji wa jamii.

Wajibu walionao Wabahá'í—kazi mnayoitekeleza katika maeneo yenu, klasta zenu na taifa lenu--ni kuwasaidia watu wote kutambua utambulisho wa pamoja kama wana wa familia moja ya binadamu na hivyo kuungana pamoja ili kujenga jamii zilizositawi kiroho na kimwili zinazodhihirisha umoja katika mchanganyiko. Kila mtu ana jukumu lake katika shughuli hii. Kila mmoja huleta vipengele bora vya utamaduni wake ndani ya mwingiliano mpana wa kijamii na kuziweka kwenye huduma ya wote, wakitupilia mbali vipengele visivyofaa kwa manufaa ya wote. Katika muktadha huu, mchanganyiko wa asili ya makabila na mila zinazotofautisha watu wa nchi yenu ni hazina inayotajirisha taifa lenu na ulimwengu. Ni baraka iliyoje kwao—kila mmoja na wote—wanapoongeza utiifu wao kwa kukumbatia maslahi muhimu ya taifa zima na ujumla wa binadamu ili, kama wana wa familia moja, waweze kusitawi na kushamiri.

*

Janga la utambulisho linahusiana moja kwa moja na kuenea kwa ubaguzi. Leo, ubaguzi wa kila aina unaenea ulimwenguni, ukiharibu dhamira za mamilioni ya watu na kumaliza nguvu zao. Unaiangamiza jamii wakati ambapo umoja ni muhimu zaidi katika kutatua matatizo ya mahali, ya kitaifa na kimataifa ambayo yanaonekana kushindikana.

Kauli katika maandiko ya Imani kuhusiana na madhara yanayotokana na ubaguzi kwa watu binafsi na kwa jamii ni yenye msisitizo mno, 'Abdu'l-Bahá amesema kwamba binadamu wanaharibika pindi wanapokuwa mateka wa njozi zao na dhana potofu. Ubaguzi huitia doa roho ya mwanadamu, unawadhalilisha wote wawili mbaguzi na muathiriwa, hutia giza mitazamo na uelewa, na huzuia ufanikishaji wa kile kiwango bora cha haki kilichotangazwa katika maandiko, ya kwamba "kuona kwa macho yako mwenyewe na siyo kwa macho ya wengine" na "kujua kwa akili yako mwenyewe na siyo kwa akili ya jirani yako." Pia 'Abdu'l-Bahá ameweka bayana kuwa chuki ni "uharibu wa hekalu la mwanadamu", "mvunjaji wa misingi ya ulimwengu wa binadamu", na ni chanzo cha "maradhi ya ulimwengu". Mpaka pale ubaguzi utakapoondolewa, “ulimwengu wa wanadamu hautaweza na hauwezi kufikia amani, usitawi na utulivu”. “Ulimwengu wa wanadamu hauwezi kuokolewa kutoka katika giza la asili na hauwezi kufikia mwangaza isipokuwa kupitia kuacha ubaguzi na kutwaa maadili ya Ufalme.”

Zingatio letu muhimu hapa, kama tulivyoeleza, ni ubaguzi wa kikabila. Kutoaminiana, hofu, chuki au kumbagua mtu mwingine au kundi lote kwa misingi ya ukabila ni ugonjwa wa

kiroho. Pia ni janga linaloathiri miundo ya kijamii na kusababisha ukosefu wa utulivu. Katika muktadha huu, kukomesha ubaguzi wa kikabila huhitaji mabadiliko katika ngazi zote mbili; ya mtu binafsi na mazingira ya kijamii. "Hatuwezi kutenganisha moyo wa binadamu kutoka kwenye mazingira yetu ya nje", Shoghi Effendi ameeleza katika barua iloyoandikwa kwa niaba yake, "na sema kwamba kila kitu kitakuwa bora pindi moja kati ya hizi ikiundwa tena. Mtu huwa hai pamoja na ulimwengu. Maisha yake ya ndani yanaunda mazingira na ni yenyewe pia yanaathirika kwa kina na yenyewe. Mmoja atende juu ya mwenzake na kila mabadiliko yanayoendana na maisha ya mtu ni matokeo ya miitikio hii ya pande zote."

Kwa mtu binafsi, kujibidiisha ili kuwa huru kutokana na ubaguzi wa kikabila ni wajibu wa msingi wa kiroho ambao hakuna mtu anayejidai kuwa ni mfuasi mtiifu wa Bahá'u'lláh anaweza kupuuza. Kumbagua mtu yeyote kwa sababu ya ukabila kwa uchungu kunakiuka roho inayohuisha Imani. "Ikiwa ubaguzi wowote kwa namna zote unapaswa kuvumiliwa," Shoghi Effendi amesema, "utakuwa ubaguzi siyo dhidi ya, bali ni kwa upendeleo wa walio wachache". Haidhuru uimara wa maoni ya umma, kamwe Mbahá'i hapaswi kutenda kwa namna ambayo inaweza kumtenga mtu yeyote. "Acha waone hakuna yeyote kama adui yao, au kama kuwatakia maradhi," 'Abdu'l-Bahá amesema, "lakini fikiri juu ya binadamu wote kama marafiki zao; watambue viumbe wageni kama wenzao, mgeni kama mshirika, kuishi huru bila ubaguzi, kutokuweka mipaka."

Juhudi za mtu binafsi katika muktadha huu lazima zianze na jitihada za bidii sana ili kukuza sifa za kiroho kama vile upendo, ukweli, wema, haki na ukarimu; kuusafisha moyo kutokana na ubinafsi, wivu na chuki; na kupatanisha akili yake na kanuni za umoja za Bahá'u'lláh. Akijitahidi kuondoa mawazo yake, maneno, na vitendo vya ubaguzi wa kikabila, mtu binafsi amebeba ubora wake mwenyewe na ubora wa watoto wote wa Mungu. Uhuru wa kutokuwa na ubaguzi ni lazima ujidhihirishe wenyewe katika nyanja zote za maisha ya mtu binafsi-akiwa faraghani na mbele ya umma, katika jumuiya za Kibahá'i, na katika jamii pana zaidi. Mazingira ya nyumbani ni lazima yawe huru na tabia, mienendo, muonekano, na ushirikiano ambao hutoa nafasi ya majivuno. Katika jamii ya Kibahá'i, Mungu amekataza kwamba ushiriki wa waumini watiifu katika mchakato wa uchaguzi wa Imani kwa kusukumwa na maslahi finyu ya kikabila, au kwamba huduma hiyo katika kamati, wakala, na asasi zichafuliwe kwa chuki na upendeleo. Katika jamii, uhuru wa muumini kutokana na chuki ni lazima udhihirike katika maeneo yote ya kijamii anayoingia—shuleni, kazini, taasisi za kitamaduni, mashirika ya kitaaluma. Wajibu wa muumini wakati wote ni kuonesha nguvu ya umoja ya mafundisho ya Bahá'u'lláh kwa kushirikiana na watu mbalimbali kwa moyo mkunjufu, upendo kamili,  na roho ya urafiki wa kweli. Kama ilivyokuwa maamrisho ya 'Abdu'l-Bahá, "Kwamba acha wale watakaokutana nawe wajue, bila wewe mwenyewe kutangaza ukweli, kwamba kwa kweli wewe ni Mbahá'í."

Kama ilivyo kwa mazingira ya kijamii, ubaguzi wa kikabila unaweza kujipenyeza katika nyanja nyingi za maisha ya pamoja na, katika hali mbaya zaidi, kujidhihirisha katika mizunguko yenye kujirudia ya mgogoro wenye vurugu kali. Ubaguzi wa kikabila mara nyingi huchochewa au huzidishwa na sababu hasi ziliizoenea katika jamii, na marafiki ni lazima watafute kupata uelewa mpana wa sababu hizi ikiwa wanataka kutoa mchango wenye maana ili kuondokana na athari zake. Fikiria, kwa mfano, madhara ya ujinga na jinsi unavyopofusha watu kwenye ukweli kwamba binadamu wote tunachangia sifa za kiroho zinazofanana, ni washirika wa familia moja ya binadamu, na wakazi wa nchi moja. Ambapo watu hawafahamu michakato ya kihistoria ambayo imeunda jamii zao, wanaweza kung'ang'ania kwa ushupavu utambulisho unaowagawa ambao unaweza kuwa na mizizi yake katika zama zilizopita za ukandamizaji. Migawanyiko ya kisiasa kati ya au ndani ya nchi, ambayo imeasisiwa na binadamu, huwa ni misingi ya ujinga wa kutoaminiana na hofu kwa makundi mengine. Pia fikiria matokeo ya tabia ya kuiga kwa

upofu na bila tafakari ya kina kuendeleza njia za fikra, mazungumzo, na mahusiano zenye kuleta mpasuko. Simulizi za historia zilizopotoshwa zinasambazwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine hutumiwa ili kueneza fikra finyu ya umiliki, ili kuhalalisha madai ya ubaguzi, ili kuchochea uhasama wa zamani au kuonyesha matukio yaliopita ambayo yanaibua hisia za uhanga. Lugha inatumika vibaya katika kupandikiza hisia hasi za kibaguzi ambazo zinabagua na kudhulumu wengine. Zingatia pia namna gani katika huduma yenye ufinyu wa maslai binafsi-iwe kisiasa au uchumi-migawanyiko inachochewa, ushindani unaanza, na migogoro kudumishwa, kwa namna gani, kimsingi, ukabila hutumiwa kama chombo katika utafutaji wa nguvu za kisiasa na faida za kiuchumi. Pia, zingatia, jinsi gani kupenda mali kunavyoongeza utofauti wa utajiri na umasikini na jinsi gani dhuluma za kiuchumi huzalisha mipasuko ambayo inazidisha chuki, hata miongoni mwa watu wale wale waliotengwa. Ushindani kwa ajili ya rasilimali chache hudhoofisha motisha kwa mtu binafsi na motisha ya pamoja na kuzalisha uhasama na wivu ambao unaharibu mahusiano.

Hizi ni baadhi ya sababu zinazounda mazingira ya kijamii ambayo ubaguzi wa kikabila hushamiri. Watu wote wenye nia njema wana wajibu wa kuongeza ufahamu wao wa mambo haya na kuimarisha uwezo wao wa kukabiliana nao. Ushawishi wa tamaduni pia unapaswa kuwa kwenye fikra. Kila tamaduni ina vipengele vingi vizuri ambavyo ni salama kwa ukuzaji wa umoja katika mchanganyiko, ambavyo lazima viimarishwe, vile vile masuala hasi yanayochangia uzalishaji wa ubaguzi, ambayo ni lazima taratibu yatelekezwe. Miingiliano yenye maana miongoni mwa watu inayoletwa kutoka makundi tofauti ya watu huchochea mazingira ambayo ndani yake ukuaji wa tamaduni yanaweza kutokea. Kuhifadhi na kukuza mila na desturi ambazo huzalisha uadui ni kikwazo cha mauti kuelekea uboreshaji wa jamii. Jumuiya ya Wabaha'i inaporwa uwezo wake wa kukuza umoja katika mchanganyiko ikiwa marafiki, kwa kujua au kutojua, huzalisha tena katika miingiliano yao na ushirika wao na jamii mielekeo ile ile inayochochea ubaguzi.

*

Hivyo basi, ni kazi gani iliyopo mbele yenu ? Namna gani mutaimarisha ruwaza ya mwingiliano unaokuza umoja katika mchanganyiko na kuondoa sababu za kijamii zinazosukuma ubaguzi ? Namna gani lengo hili linahusiana na jitihada zenu za sasa ili kuijenga jumuiya mahiri na, kwa upana zaidi, kuchangia kwenye ustawi wa kiroho na kimwili wa jamii yenu ?

Shoghi Effendi alitoa wito kwa marafiki "kufikia vilele vya juu zaidi vya ushujaa wa ubora sambamba na ubinadamu unavyotumbukia katika kina cha kukata tamaa, mmong'onyoko, mafarakano na dhiki". Mipango ya kiulimwengu inalenga kukuza uwezo wa kila kundi la binadamu kukabiliana na nguvu hasi za kijamii kwa kuchangia kwenye ustawi kupitia matumizi ya mafundisho ya Imani. Kadiri Mipango inavyoendelea kufunguka, michakato yake taratibu itadhihirisha uwezo wake wa kuzuia kila chombo kilichoundwa na binadamu kwa kipindi kirefu cha utoto wake kwa kundi moja kudhulumu lingine na kwa kuendeleza mgogoro na mfarakano. Hiki ni kiini cha kazi munayoendelea kufanya katika jumuiya zenu. Juhudi zenu katika eneo la ujenzi wa jamii, kitendo cha kijamii, na mjadala wa hadharani huwakilisha njia za kuamsha nguvu zilizofichwa ndani ya nafsi ya mwanadamu na kuzielekeza kuelekea uboreshaji wa jamii.

Jitihada zenu za kupeleka ujumbe wa Imani kwa makundi mbalimbali ya kijamii hukuza msingi wa ushirika wa mwingiliano wakikabila na kitamaduni. Wanaunda ushirikiano na msaada wa pamoja baina aya watu wenye asili mbalimbali ni tabia ya kipekee ya maisha ya jamii ya waBaha'i. Munatafuta, katika hili, kuonyesha kwamba tabia kuu ya Wabahá'i ya kuwa

na muonekano halisi wa nje, muwazi huru kwa wote, na mjumuikaji thabiti. Umakinifu wenu katika kuimarisha uwezo wa kusoma maandiko ya Imani umewezesha idadi kubwa kuwahi kutokea ya kuunda mahusiano ya kijamii yanayoakisi viwango na kanuni za Kibahá'i. Hii inaimarisha kwa washiriki wote shauku na uwezo wa kujitoa kwa vitendo vya huduma isiyovutia kwa jamii na kutakasa nia zao kwa kadiri wanavyojifunza kujitolea dhabihu kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa wote. Kujitoa kwenu kwa mtindo wa utendaji uliojikita katika mafunzo endelevu, majadiliano, utendaji, na tafakari umesaidia kuwakomboa watu binafsi na jamii kutokana na kuiga kwa upofu na kuweka nanga juhudi za wazi za ujifunzaji ili kuanzisha “misingi mipya kwa furaha ya binadamu". Nguvu munazotoa kwa elimu ya kiroho ya watoto na kwa uwezeshaji wa kiroho wa vijana chipukizi husaidia rika chipukizi kuweka misingi ya tabia bora, huwakinga dhidi ya doa la ubaguzi, na uongoza uwezo wao unaoibuka kuelekea huduma kwa jamii. Mkazo munaoweka kwenye familia hubadilisha kiini hiki cha msingi cha jamii katika nafasi ambapo vijana wanaweza kujiingiza roho ya umoja na kuepuka mielekeo yote inayoleta mgawanyiko. Juhudi zenu za kujenga uwezo wa kutumia kanuni za kiroho na maarifa ya kisayansi katika uboreshaji wa hali ya kijamii na kiuchumi husaidia watu kukabiliana na dhuluma za kiuchumi kupitia kitendo cha pamoja bila kukimbilia kwenye mizozo. Michango yenu katika vikao vingi ambapo mazungumzo kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii hufanyika huimarisha uwezo wa pamoja wa mazungumzo ya juu na husaidia watendaji mbalimbali kufikia umoja wa mawazo na vitendo, kwa kuchota kwenye mafundisho na uzoefu wa Kibahá'i. Nafasi ya kati muliyoipa mashauriano huongeza uwezo wa utafutaji wa pamoja wa ukweli, huachilia huru michakato ya kufanya maamuzi kutokana na mabishano na mielekeo pinzani, na kuwawezesha watu kutoka asili mbalimbali hadi kuvuka tofauti na kusawazisha maoni. Michakato ya chaguzi na ya kiutawala inajenga muundo wa fkra na mwenendo ambao utakomboa uongozi na utawala kutokana na masilai binafsi na rushwa zinazohusika. Kwa kujibidiisha ili kutanua msingi wa ushiriki katika nyanja zote za maisha ya jamii yako, munajenga hali ambayo watu binafsi kutoka makundi mbalimbali ya kijamii wanaheshimu umoja wao wa ubinadamu, wanatambua masilai yao ya pamoja, na kujenga muono wa mustakabali wao wa pamoja. Ushiriki kama huu huimarisha mahusiano ya kijamii kama nafsi zinazohudumu bega kwa bega kwa asili ya ubora wa jamii. Haijalishi ukubwa au udogo, wa jamii yako –juhudi za kujenga zimeelekezwa katika kukuza kiini na ruwaza ya utaratibu wa dunia mpya kwa kuanzisha aina ya mahusiano ambayo imeangaziwa kutoka kwa Bahá'u'llah. Na miongoni mwa wale wote wanaofanya kazi pamoja huibuka lugha inayoinua wote na kutomdharau yeyote, lugha ambayo ina uwezo wa kuunganisha mioyo na kifungo kisichoweza kufutwa cha upendo na uwezo wa kuungana roho katika harakati za pamoja za jamii ambayo inaweza kuwa kama bustani moja iliyojaa maua ya umbo mbalimbali, rangi na manukato yote. Ni kwa njia hizi zote ambapo munaunda jumuiya mpya ambazo zinazoweza kutumika kama kielelezo cha kuigwa na uhusiano unaowawezesha kuwa kama chachu ya mabadiliko ya maisha ndani ya Taifa lenu.

*

Marafiki wapendwa katika taifa hili kubwa la Kiafrika! Tunajua kwamba hali za mizozo ya kijamii ambamo munafanya kazi wakati mwingine zinasumbua na kukatisha tamaa. Kaka na dada zenu katika nchi nyingine nyingi pia hukabiliana na hali kama na hizo. Ingawa wakati mwingine inaweza kuonekana kuwa tumaini la jamii inayo unganika kiuhalisia hupungua siku baada ya siku, wakati migogoro iliyojengwa na ubaguzi ikijiridia mara kwa mara na kuongezeka, jukumu lenu lazima ibaki lieleweke daima, muonekano wenu wenye kujiamini daima, kujitoa kwenu kuwe imara daima. Muna uwezo wa kuunganisha maelfu na maelfu ya mioyo. Enyi wanaopaza wimbo wa umoja katika mchanganyiko, ni lazima, muwe kwa maneno na matendo nembo zake. Ikiwa matendo yenu yana akisi mwelekeo uliopo katika jamii, ikiwa mutapuuzia misingi ya imani yenu, nini kitakachobaki basi? Chumvi itakuwa imepoteza ladha

yake. Wekeni kando vikwazo vyote, kiakili au vinginevyo, na hivyo pelekeni ushindi wa kweli kwa ajili ya umoja wa ubinadamu kwa Bwana mwenye upendo katika miaka hii tisa,.

Kwa kumalizia, sasa tunawahubiria vijana: Mustakabali wa baadae upo mikononi mwako. Usifanye makosa, munajenga hekalu ambalo litakua kimbilio la watu wenu juu ya misingi iliyowekwa na mama zenu na baba zenu. Maendeleo endelevu yatategemea kujitolea kwenu katika kujenga umoja wa kweli na kiwango ambacho munaimarisha mazoezi yenu ya nidhamu hizi za kiroho zilizowekwa na Bahá'u'llah ambazo zitawasaidia kung'arisha vioo vya mioyo yenu ili ziakisi sifa za Mungu. Ni matumaini yetu kwamba mutaimarisha miongoni mwenu mahusiano ya kiroho yatakayo zuia nguvu ya ubaguzi. Acheni mfano wa 'Abdu'l-Bahá uwe muongozo wenu-namna alivyoishi maisha Yake kama Dhabihu ya kila siku kwa sababu ya umoja wa ubinadamu, namna Alivyokumbatia mapenzi yasiyo na ubinafsi kwa watu wote waliokatiza katika njia Yake, namna alivyoona iliakisi sura ya Mungu mwenye upendo katika kila nafsi. Hivyo, pia, mtawaona wenzi wenu wote. "Katika zama hizi angavu", Alisema, "kwamba ambayo imethibitishwa ni umoja wa ulimwengu wa binadamu. Kila nafsi iliyohudumu katika umoja huu bila shaka watasaidiwa na kuthibitishwa." Tunathamini matumaini kwamba, katika juhudi zenu za kutafuta washiriki wa maisha, mtapinga kila ushawishi utakaotoa umuhimu wa msingi kwa ukabila, kwamba makazi ambapo kila nafsi itakaribishwa, na mutawalea watoto ambao watakuwa mabingwa wa umoja. Tuna hakika kwamba katika maisha ya taifa lenu, mtang'ara kama watu wa kutumainiwa kwa wote, kama watumishi wa wote, kama viunganishi kwa wote. Acha matendo yenu yaandike sura ifuatayo katika historia ya nchi yenu, moja ambayo itakuwa huru kutokana na na ubaguzi na mizozo. Kwa hivyo raia wenu, kila mmoja kama mto mkuu, watatiririka katika bahari kuu ambyo maji ya uzima itajaa katika bahari ya familia moja ya binadamu.

Tunaelekeza sala zetu kwa Uzuri Uliobarikiwa kwenye Kizingiti Kitakatifu cha kaburi lake ili Aweze kuunganisha kwa uthabiti zaidi katika upendo raia wa taifa lenu mlipendalo sana.

[Sahini: Nyumba ya Haki ya Ulimwengu]